## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## MIFUMO YA TEHAMA YA TAASISI ZA UMMA KUBADILISHANA TAARIFA KIDIJITALI

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Ndugu Wanahabari,**

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019, ikiwa na majukumu ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao, pamoja na kusimamia uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma.

Miongoni mwa jitihada hizo ni kuhakikisha Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi za Umma inawasiliana na kubadilishana taarifa ambapo, Mamlaka imejenga Mifumo ifuatayo inayowezesha Mifumo ya TEHAMA Serikalini kubadilishana taarifa.

### 1. Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (GovESB)

Mamlaka imefanikiwa kujenga Mfumo unaowezesha mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa, ujulikanao kama ***Government Enterprises Service Bus*** **(GovESB)**. Mfumo huu, umetengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuzingatia kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, kinachoitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao, kuanzisha na kuendesha Mfumo unaowezesha mifumo ya TEHAMA Serikalini kuwasiliana na kubadilishana taarifa.

Sambamba na kutekeleza matakwa hayo ya kisheria, pia ujenzi wa Mfumo wa GoVESB ni utekelezaji wa agizo la **Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, la kuhakikisha mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma inaunganishwa na kubadilishana taarifa.

**Ndugu Wanahabari,**

Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (*Government Enterprise Service Bus*-GovESB), ni mfumo wa kielektroniki unaounganisha mifumo ya TEHAMA ya taasisi za umma iweze kusomana na kubadilishana taarifa kila inapohitajika. Lengo la Mfumo huu ni kuziwezesha taasisi za umma kubadilishana taarifa kidijitali kwa usalama, kupunguza urudufu wa mifumo, kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, kupunguza gharama za uendeshaji pamoja na kuokoa muda kwakuwa taarifa hupatikana kwa wakati.

**Ndugu wanahabari,**

Kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo wa GovESB, kulikuwa na changamoto mbalimbali za ubadilishanaji wa taarifa katika taasisi za umma, zikiwemo kutumia muda mrefu kupata taarifa kwani, taasisi zililazimika kuwasilisha maombi ya kupata taarifa inazohitaji kwa njia ya barua katika taasisi husika. Utaratibu huu wa barua ulichukua muda mrefu kupata taarifa hizo, jambo lililochangia kupunguza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Changamoto nyingine, ilikuwa ni utofauti wa utaratibu wa kupata taarifa kutoka taasisi moja hadi nyingine, kwani kila taasisi inao utaratibu wake wa ndani wa kupata na kutoa taarifa na wakati mwingine utaratibu hubadilika.

Hapo, awali ili mifumo ya TEHAMA iweze kusomana, ililazimika kuunganisha mfumo mmoja kuzungumza na mifumo mingine kila inapohitajika yaani "*point-to-point connections".* Uunganiswaji huu ulisababisha urudufu wa mifumo, kupungua kwa usalama, kupunguza ufanisi wa mifumo na kuongeza gharama za usimamizi na uendeshaji wa mifumo ya TEHAMA.

Kupitia GovESB, changamoto hizo zimetatuliwa na sasa taasisi zote zinazobadilishana taarifa kupitia GovESB hupata taarifa zinazohitaji kwa wakati na kwa usalama zaidi. Vilevile, Mfumo huu umesaidia kuokoa muda wa kuwahudumia wananchi, lakini pia kupunguza gharama za kutengeneza mifumo midogo midogo ya TEHAMA inayounganisha na mifumo ya taasisi nyingine.

**Ndugu wanahabari,**

Hadi sasa jumla ya Taasisi za Umma 109 zimeunganishwa katika mfumo wa GovESB na mifumo 117 imesajiliwa. Miongoni mwa taasisi hizo ni Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wakala wa Leseni za Biashara (BRELLA), Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), n.k.

**Ndugu wanahabari,**

Mfumo wa GovESB umeleta mafanikio makubwa katika sekta za elimu na sheria kwani taasisi nyingi katika sekta hizo zinabadilishana taarifa kupitia GovESB. Kwa upande wa sekta ya sheria, taasisi zinazobadilishana taarifa ni Mahakama, Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka (NPS). Hivyo mfumo huu umesaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, uwazi pamoja na utoaji haki kwa wananchi kwa wakati.

Katika sekta ya elimu, Taasisi zilizounganishwa na kubadilishana taarifa kupitia mfumo huu ni Pamoja na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), nk.

Ili kuhakikisha Taasisi nyingi zaidi zinajiunga na mfumo wa GovESB na kubadilishana taarifa, e-GA imekuwa na mikakati madhubuti ikiwemo, kufanya vikao na taasisi mbalimbali ambapo kati ya Agosti na Novemba 2023, eGA imefanya vikao na Taasisi 55.

2. **Mfumo wa Pamoja wa Kielekroniki wa Uondoshaji wa Shehena maeneo ya forodha (*Tanzania Electronic Single Window System - TeSWS*).**

**Ndugu Wanahabari,**

e-GA imeshirikiana na Taasisi nyingine za Umma ikiwemo TRA, TPA na Wizara ya Fedha katika kusanifu Mfumo wa Pamoja wa Kielekroniki wa Uondoshaji wa Shehena maeneo ya forodha (***Tanzania Electronic Single Window System - TeSWS***). Mfumo huu ni moja ya miradi inayotekelezwa, chini ya mradi mkubwa wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kukusanya Mapato ya Ndani na Usimamizi wa Mali Asilia (*Institution Support Project on Domestic Resources Mobilisation and Natural Resources Governance-ISP-DRM-NRG*), unaosimamiwa na Wizara ya Nishati.

Mfumo wa TeSWS ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa kuboresha Mazingira ya Biashara nchini – MKUMBI ***(Blueprint)***. Mfumo huu unawawezesha wafanyabiashara kukamilisha maombi ya vibali na maandalizi ya malipo ya kodi za forodha kidijitali bila kwenda kwenye Taasisi mbalimbali za udhibiti wa forodha, hivyo kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Mfumo wa TeSWS unaruhusu wadau wa biashara na wasafirishaji kuwasilisha mara moja tu kwenye mfumo taarifa za kiforodha na shehena zinazoingia na kutoka nchini, pamoja na zile zinazopita nchini kwenda nchi jirani ambapo kila mdau husika ataziona na kuzifanyia kazi kwenye mfumo.

Ujenzi wa Mfumo huu unaratibiwa na e-GA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Wizara ya Fedha, pamoja na Taasisi za Serikali za Udhibiti kama vile Shirika la Viwango Tanzania (TBS), nk.

**Ndugu wanahabari,**

**Mfumo wa TeSWS** una awamu tatu: Awamu ya Kwanza inahusu moduli za taratibu za forodha **"Customs Procedures"** na zile za taasisi za Uthibiti na Ukaguzi, na Malipo ya Huduma. Awamu hii inatumika tayari kwa Bandari ya Dar Es Salaam na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ambapo kampuni za wakala wa forodha (CFA) **1,496** kati ya **1,496** sawa na asilimia **100** pamoja na makampuni ya watunza shehena **246** zinatumia mfumo huu.

Awamu ya pili inahusu moduli za taratibu za ujio wa meli na uondoshaji wa shehena Maeneo ya forodha **"Cargo Management",** awamu hii ya mfumo wa TeSWS imeanza kutumika kwa Bandari ya Dar Es Salaam kwa Wakala wa Meli na *Consolidators*, na imewezesha kuunganisha na kubadilishana taarifa kati ya mifumo ya TRA (Tanzania Custom Integrated System - TANCIS) na TPA (Terminal Operating System – TOS). Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kuhusu kusomana kwa mifumo ya TPA na TRA.

Na awamu ya tatu inahusu moduli za taratibu nyingine ndogondogo za forodha ndani ya TRA, TPA, Posta na Viwanja vya Ndege. Awamu hii ipo katika majaribio ya ufundi na watumiaji.

3. **Ubadilishanaji wa Taarifa Kati ya Mifumo ya TEHAMA ya Serikali na ya Sekta Binafsi**

**Ndugu wanahabari,**

Ubadilishanaji wa taarifa kati ya mifumo ya Serikali na ya Sekta binafsi, unawezeshwa kadiri ya mahitaji yanavyojitokeza. Mathalani,mfumo wa malipo ya Serikali (GePG) umeunganishwa na Benki zote nchini pamoja na Kampuni zote za Simu  za Mikononi (Mobile Network Operators- MNOs), ili kuwezesha huduma ya malipo ya Serikali kupitia simu za mikononi. Aidha, Mfumo wa huduma za Serikali kupitia simu za mkononi (*Government Mobile Platform* - mGov) umeunganishwa na mifumo ya kampuni zote za simu nchini hivyo kuwezesha kutoa huduma za Serikali, kwa njia ya simu za mkononi. Mifumo ya Serikali kubadilishana taarifa na mifumo ya sekta binafsi ni kazi iliyofanyika na inaendelea kufanyika kadri ya mahitaji.

**Ndugu wanahabari,**

Mamlaka ya Serikali Mtandao, ipo tayari muda wowote kufanya kazi na taasisi zote za umma kuhakikisha taasisi hizo zinajiunga na kubadilishana taarifa kupitia GovESB, hivyo nitoe wito kwa taasisi zote ambazo bado hazijajiunga, kuwasiliana na e-GA ili ziweze kuunganishwa. Aidha, upo utararibu wa kuwezesha mifumo ya taasisi za sekta binafsi inayohitaji kubadilishana taarifa na mifumo ya Serikali na kazi hii itaendelea kutekelezwa kadiri ya mahitaji.

**Imetolewa Na:**



**Eng. BENEDICT NDOMBA**
**MKURUGENZI MKUU**
**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**
**Disemba 22, 2023**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255 26 2961957, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
*"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"*